JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA TISA

29 JUNI 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 29 JUNI, 2010

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

131. MHESHIMIWA EMMANUEL JUMANNE LUHAHULA (BUKOMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kuwajengea uwezo Viongozi wa Serikali katika ngazi zote ni jambo zuri katika kuleta utawala bora:-

(a) Je, nani anawajibika kutoa elimu na semina kwa Wenyeviti wa Vitongoji na Serikali za Vijiji katika maeneo husika;

(b) Je, katika Wilaya ya Bukombe semina za Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji zimefanyika mara ngapi tangu waingie madarakani mwaka 2004.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:

132. MHESHIMIWA MWANNE ISMAIL MCHEMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma:- Katika ajira ya Mtumishi wa kada ya Katibu Muhtasi (Personal Secretary)

inamlazimu awe na cheti cha shorthand/hatimkato ndipo aweze kuajiriwa au kupandishwa cheo; lakini hivi sasa huduma hizo hazitumiki kutokana na sayansi ya utandawazi inayomtaka mtumishi kujua *Computer Stage One* na *Stage two* au zaidi:-

Je, Serikali iko tayari kufanya marekebisho kwa kufuta ulazima huo ambao ni wa muda mrefu ili kwenda na wakati.

133. MHESHIMIWA MWINCHOUM ABDULRAHAMAN MSOMI (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma:- Imekuwa ni kawaida ya Serikali kuwahamisha watumishi wake kutoka kituo kimoja kwenda kingine; zoezi ambalo hufanyika hata kwa watumishi wa ngazi ya Tarafa, Kata na Vijiji; ingawa yapo malalamiko katika ngazi hizo kuwa hawajalipwa fedha zao za uhamisho:-

(a) Je, ni watumishi wangapi ambao hawajalipwa fedha zao za uhamisho hadi sasa;

(b) Je, ni sababu gani zinazosababisha wasilipwe fedha zao kwa wakati husika.

WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:

134. MHESHIMIWA FAIDA MOHAMMED BAKAR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana:- Baadhi ya wafanyakazi wa Viwandani, Machimboni, Mashamba makubwa na sehemu nyingine za sekta binafsi hupata athari kubwa sana zinazotokana na mazingira mabaya ya sehemu za kazi kama vile kupata ajali katika viungo vyao vya mwili, kuchubuka ngozi kutokana na kemikali, kupofuka macho n.k wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kikazi:-

Je, ni fidia gani wanalipwa wafanyakazi hao pindi wanapopata athari hizo wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kikazi.

135. MHESHIMIWA WILLIAM HEZEKIA SHELLUKINDO (BUMBULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana:- Kuongeza ajira nchini ni eneo mojawapo la utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM):-

(a) Je, ni maeneo gani ambayo yameongeza ajira kiasilimia;

(b) Je, nafasi za Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Mtaa, Mwenyekiti wa Kijiji, Udiwani, Ubunge, Uwaziri na Urais ni miongoni mwa ajira hizo

zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi;

(c) Je, ni ajira gani zenye mvuto zaidi kwa Watanzania.

WIZARA YA MIUNDOMBINU:

136. MHESHIMIWA PHILEMON NDESAMBURO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu:- Watalii wengi huanzia utalii nchini Kenya na hasa Mombasa na baadaye kuja Tanzania lakini wengi wa watalii ambao hao hupenda kuja kuuona na kuupanda Mlima Kilimanjaro hukatishwa tamaa na mzunguko wa kupitia Nairobi na Namanga:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuendeleza usafiri wa Reli kutoka Mombasa kuja Moshi ili kuvutia watalii wengi kuja Moshi.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

137. MHESHIMIWA JOB YUSTINO NDUGAI (KONGWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Katika Mkutano wa **CITES** ulifanyika Doha mwaka huu (2010) Tanzania iliomba kuuza sehemu yake ya pembe za Ndovu zilizojaa kwenye Ivory Room Dar es Salaam lakini ombi hilo halikukubaliwa:-

Je, Serikali inawaambia nini Watanzania juu ya hatma ya pembe hizo.

138. MHESHIMIWA DKT. CHRISANT MAJIYATANGA MZINDAKAYA (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali inafahamu kuwa, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuna vivutio vya kuiwezesha nchi kuendeleza utalii lakini havitumiki kwa ukamilifu kuisaidia nchi kujipatia mapato kutokana na utalii.

WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

139. MHESHIMIWA CHARLES NDELIANARUWA KEENJA (UBUNGO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Utaalamu wa kisasa wa uzalishaji wa viumbe “bio-technolgy” una manufaa makubwa katika kuongeza uzalishaji, ukinzani wa magonjwa, ubora wa mazao n.k:

(a) Je, ni lini Serikali itaandaa Sera, Sheria na Kanuni za kusimamia uingizaji wa teknolojia hiyo na itaingizwa lini nchini;

(b) Kumekuwa na hofu kwamba teknolojia hiyo inaweza kuwa na madhara; Je, ni madhara gani hayo, na kama yapo ushahidi gani unaothibitisha kutokea kwa madhara hayo;

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

140. MHESHIMIWA SHOKA KHAMIS JUMA (MICHEWENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Tanzania inategemea wahisani katika Bajeti yake ya Maendeleo kwa asilimia kubwa:-

Je, Serikali imejipanga vipi ili kujinasua katika hali hiyo ya kutegemea wahisani.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA
29 JUNI, 2010

DKT. T.D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE